NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

4 Januari 2022

Kwa Wabahá'í wa Ulimwengu

Marafiki Wapendwa sana,

Wakati huu tupo pamoja na kundi la Washauri wa Bara—wengi wao wapo hapa Nchi Takatifu, ambapo baadhi ambao hawakuweza kuja hapa wanashiriki kutokea mbali—na siku ya sita na ya mwisho ya kongamano lao, lililomakinikia juu ya Mpango ujao wa Miaka Tisa, inapokaribia kuhitimishwa. Yapo mengi sana yanayoweza kushirikishwa nanyi kuhusiana na ari ya kongamano hili, kama ionekanavyo kwa washiriki wake. Wakibobea katika tajiriba, wamekuwa mashuhuda kwenye uinukaji wa uwezo katika ulimwengu wa Kibahá'í, na wanafurikwa na imani kuhusu kile mnachoweza kukitimiza zaidi. Tusingependelea upataji wa uelewa hodari na wenye umaizi zaidi wa kile kinachoongelewa katika Mpango ufuatao kuliko kilichodhihirishwa katika mashauriano ya roho hizi zilizojiweka wakfu. Lakini huu, bila shaka, ni mwanzo tu. Wakati Washauri watakaporejea kwenye nchi za mabara matano,watawaletea ninyi na wale wanaohudumu pamoja nanyi yale yote waliyoyapata. Wao pamoja na wasaidizi wao watakuwa pamoja nanyi wakati mnapojiandaa kwa ajili ya shughuli hii kuu ya pamoja—hususan kupitia ushiriki wenu katika wimbi la makongamano ya hivi karibuni yanayoenda kuukumba ulimwengu wote, ambapo miito ya Bahá'u'lláh ya kufanyakazi kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu itauamsha mkusanyiko wa watakia heri wa binadamu.

Muunganiko wa hali katika ulimwenguni kwa jumla na ndani ya Imani umeufanya huu kuwa wakati wenye nguvu maalum. Changamoto za kiulimwengu zinazoikabili jamii ya binadamu hivi sasa ni jaribu kali la utayari wake wa kuweka kando maslahi binafsi ya muda mfupi na kufikia vipindi vyenye uhalisia wa umakinifu huu bora wa kiroho na kimaadili: kuna familia moja tu iliyounganika ya jamii ya binadamu na inashiriki makazi mamoja ya thamani. Wakati huu huu, wafuasi wa Bahá'u'lláh wanatathmini upya uwezekano mbalimbali uliopo mbele yao wa kuachilia nguvu ya Imani ya ujenzi wa jamii. Mpango huu utaujaribu ustahimilivu wao, utashi wao na nguvu ya upendo wao kwa wale waishio kando yao. Watasaidia kuzilea, kila mahali, jumuiya zenye kusudi moja ambazo hutambua nguvu ya umoja katika kuponya, kuvuka mipaka ya uwezo wa kibinadamu. Ndani ya jumuiya hizi, kila roho inaweza kupata kimbilio, na katika jitihada nyingi za marafiki kwa ajili ya kusali na kuabudu, kwa ajili ya elimu, kwa ajili ya mabadiliko ya kijamii, kwa ajili ya maendeleo ya jumuiya—katika yote haya, kila roho inaweza kupata nafasi ya kukua na kuhudumu. Tunaimarishwa na ahadi ya 'Abdu'l-Bahá: "Wadogo watafanywa kuwa wakubwa, na wanyonge watapewa nguvu; wale wenye umri mdogo watakuwa watoto wa Ufalme, na wale waliokengeuka wataongozwa kwenye makazi yao ya mbinguni."

Wakati Bahá'u'lláh alipotuma habari Zake njema za furaha, waumini waliojifunga ambao wangebeba ujumbe Wake kwenda kwa binadamu kwa idadi walikuwa wachache sana. Leo, sifa ziwe kwa Mungu, kujitoa kwa marafiki kumekuwa dhahiri na idadi yao imepaa. Mioyo yao na ithibitishwe kupitia uwezo wa Neno Lake na, kwa kila tukio na kwa kila nafasi, waweze kung'aa kwa mwanga wa wangavu wa mbinguni. Hiyo ndiyo itakuwa sala kwenye ndimi zetu

na matumaini katika vifua vyetu wakati, leo hii, tukiwa pamoja na Washauri, tunaingia katika Kaburi Takatifu la Uzuri Uliobarikiwa ili kuomba kwa niaba yenu.

Imesainiwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu